

## GRADE 4 END TERM 1 AUGUST 2021 KISWAHILI

### ZOEZI LA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amwamkue mwanafunzi na kumwomba akae. Mwalimu ajitambulishe.

"Mimi ni mwalimu \_\_\_\_\_ Niambie jina lako."

"Leo ningependa tuzungumze kuhusu sokoni."

1. Sokoni ni mahali pa shughuli gani?
2. Taja bidhaa zinazoweza kupatikana sokoni.
3. Nyumbani, siku rasmi ya soko huwa lini?
4. Je, ni kina nani huweza kupatikana sokoni?
5. Bidhaa hupangwa vipi sokoni?

Alama	
	5

### ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI.

Tumbokarai alipopata habari kuwa sherehe ilikuwa imeanza, hakisubiri. Bila hata viatu, aliuchukua mkebe wake mchafu na kuanza safari. Alipofika shereheni, alienda moja kwa moja hadi jikoni na kuwaagiza wapishi kumpakulia chakula. Alipopewa wali, aliula wote haraka na kuagiza supu ya nyama. Kila alichogiza alitiliwa katika mkebe wake mchafu. Baada ya kula kila aina ya chakula, aliketi na kushindwa kupumua. Lol! Ulafi ulimwua fisil

Alama	
	10

### ZOEZI LA 3: KUSOMA KWA UFAHAMU.

i) Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.

Vipepeo humvutia sana Rembo. Yeye hupenda kucheza nao. Kila awaonapo, yeye huacha kila anachofanya na kuwafuata. Wakati mwingine, vipepeo huruka juu zaidi na kumwacha na huzuni. Akimkamata mmoja, yeye humfunga mguuni kwa uzi na kuanza kucheza naye. Asichojua ni kuwa, vipepeo hao wanaweza kufa kwa njaa na maumivu. Daima, kaka yake humshauri asiwaumize wadudu hao lakini Rembo huwa hasikii. Vipepeo ni wadudu wapole wasio na madhara yoyote. Hatufai kuwaumiza hata kidogo.

1. Mtoto aliyetajwa kwenye hadithi anaitwa \_\_\_\_\_
2. Mtoto huyo akiwaona vipepeo, \_\_\_\_\_
3. Vipepeo wakiruka juu zaidi, msichana aliyetajwa huachwa na \_\_\_\_\_
4. Vipepeo hufungwa miguuni kwa kutumia \_\_\_\_\_
5. Je, ni nani alisema vipepeo wasiumizwe? \_\_\_\_\_

ii) Tangu kitambo, ugonjwa wa Ukimwi umekuwa tishio kubwa kwa binadamu. Ukimwi humanisha upungufu wa kinga mwilini. Ni ugonjwa ambao hauchagui umri, kabila wala tabaka. Huweza kumpata yeyote yule. Ugonjwa huu huweza kusambazwa kwa njia nyingi kama vile kugusa damu yenye virusi kwa mikono mitupu na kuongezwa damu

yenye virusi. Ukimwi hauwezi kusambazwa kwa kula pamoja au kulala pamoja na wahasiriwa. Ugonjwa huu hauna tiba. Ni vizuri kila mmoja ajilinde ili asiambukizwe wala kuambukizana Ukimwi.

6. Ukimwi humaanisha \_\_\_\_\_
7. Ugonjwa wa Ukimwi hauchagui \_\_\_\_\_ wala \_\_\_\_\_
8. Ukimwi huweza kusambazwa kwa njia nyingi kama \_\_\_\_\_
9. Tumeambiwa kwamba Ukimwi hauwezi kusambazwa tukifanya nini? \_\_\_\_\_
10. Kwa sababu ugonjwa huu hauna tiba, ni vizuri kila mmoja \_\_\_\_\_

#### **ZOEZI LA 4: SARUFI**

***Chagua neno sahihi kujazia pengo.***

damu	nyama	ladha	Mboga	magonjwa
------	-------	-------	-------	----------

\_\_\_\_\_ aina ya mchicha hunifurahisha sana. Nina \_\_\_\_\_ zila mimi hufurahia \_\_\_\_\_  
 11  
 \_\_\_\_\_ yake nzuri. Si hayo tu, mchicha pia huongeza \_\_\_\_\_ mwilini na \_\_\_\_\_  
 12  
 kutukinga tusipate \_\_\_\_\_ kama vile safura. Mchicha huweza kutayarishwa \_\_\_\_\_  
 13  
 pamoja na \_\_\_\_\_ au dagaa. Mara nyingi, mchicha huliwa kwa ugali.  
 14  
 15

***Pigia mistari vivumishi katika sentensi hizi.***

16. Mbuzi mgonjwa amelala chini ya mti.
  17. Karatasi aliyoleta ni nyeupe sana.
  18. Wao walikimbizwa na mbwa wakali.
- Tumia "ndani ya" au "nje ya" kwa ufasaha.***
19. Aliirusha peremende \_\_\_\_\_ mdomo akaimeza.
  20. Wanafunzi wameketi \_\_\_\_\_ darasa wakiota jua.

21. Kombo alikitia kitabu \_\_\_\_\_ mkoba akaondoka.
  22. Mti mrefu umemea \_\_\_\_\_ nyumba yetu.
- Andika wingi wa sentensi hizi katika wakati ujao.***
23. Alibeba mzigo mzito.  
\_\_\_\_\_
  24. Anapanda mti shambani.  
\_\_\_\_\_
  25. Amekuja na kikombe kipya.  
\_\_\_\_\_